

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



**TAARIFA KWA UMMA**

Septemba 19, 2023

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA IMEPOKEA FEDHA YA KUTEKELEZA MIRADI  
MBALIMBALI YA KIMAENDELEO NA TAYARI UTEKELEZAJI WA MIRADI HIYO UMEANZA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Mhe. Victoria Mwanziva, ametuma salamu za shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia fedha Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ya Kutekeleza miradi mbalimbali yakimaendeleo kiasi cha shilingi Bilioni **1,384,000,000.00**

Fedha hizo zimeganywa kama ifuatavyo:-

1. Ukamilishaji wa Zahanati ya Sagalu kiasi cha shilingi Milioni **50,000,000.00** na Ukamilishaji wa Zahanati ya Mbugani kiasi cha shilingi **50,000,000.00**
2. Ununuzi wa vifaa tiba kwa Zahanati ya Chimbo shilingi **33,333,333.33**, Zahanati ya Ndowa **33,333,333.33** na Zahanati ya Lihunji imepokea shilingi Milioni **33,333,333.33**
3. Vituo vya Afya vinavyojengwa vinavyohitaji vifaa tiba, Kituo cha Afya Mundindi kimepokea fedha kiasi cha shilingi Milioni **150,000,000.00** na Kituo cha Afya Luilo kimepokea fedha kiasi cha shilingi **150,000,000.00**
4. Jengo la Utawala limepokea fedha kiasi cha shilingi Milioni **50,000,000.00**
5. Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi Milioni **400,000,000.00** kwaajili ya ununuzi wa Boti
6. Ukarabati wa shule Kongwe za msingi ambazo ni shule ya Msingi Makonde imepokea fedha kiasi cha shilingi **90,000,000.00** na shule ya msingi Mavala imepokea fedha kiasi cha shilingi **90,000,000.00**
7. Ujenzi wa matundu ya vyoo kwa shule za msingi, shule ya msingi Songambebe imepokea fedha kiasi cha shilingi Milioni **10,000,000.00**, shule ya msingi Lugumbiro imepokea fedha kiasi cha shilingi Milioni **10,000,000.00** na shule ya Msingi Lipangala imepokea fedha kiasi cha shilingi Milioni **8,000,000.00**
8. Shule za sekondari zilizopokea fedha kwaajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kidato cha tano na kidato cha sita ni shule ya sekondari Chief Kidulile shilingi Milioni **88,000,000.00**, shule ya Sekondari Lugarawa shilingi Milioni **125,000,000.00** na shule ya Sekondari Mchuchuma shilingi Milioni **125,000,000.00**
9. Shule za sekondari zilizopokea fedha kwaajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo kwa kidato cha tano na kidato cha sita, Shule ya Sekondari Chief Kidulile imepokea Milioni **8,000,000.00** shule ya sekondari Lugarawa imepokea Milioni **10,000,000.00** na shule ya sekondari Mchuchuma imepokea Milioni **20,000,000.00**  
Shule ya Mundindi Elimu Maalum imepokea Milioni **30,000,000.00** kwaajili ya ujenzi wa Uzio.

Chrispin B. Kalinga

**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini (W)**  
**LUDEWA.**

***Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Makaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.***